**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Shule ya Sekondari Kirando**
**S.L.P 107**
**NAMANYERE-NKASI**
**Tarehe 06.05.2026**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIRANDO HALMASHAURI YA WILAYA NKASI MKOA RUKWA**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii na atasoma tahasusi ya _________(Aliyopangiwa na serikali ).

Shule ya Sekondari Kirando ipo umbali wa Kilometa 63 Magharibi mwa Mji wa Namanyere Usafiri wa basi kutoka mjini Sumbawanga/Namanyere unapatikana katika kituo cha mabasi Sumbawanga na Namanyere Nauli ni Shilingi **12,000/=** kutoka Sumbawanga na Shilingi **7,000/=** kutoka Namanyere,Anayetokea Mpanda ashukie Namanyere hapo atasubiri gari za kutoka Sumbawanga.na akifika stendi ya Kirando atapanda bodaboda kuja shuleni nauli ni Tsh 2,000/= tu.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe …………( Iliyotangazwa na serikali ) hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe tajwa, Mwisho wa kuripoti ni wiki mbili tu kuanzia tarehe pangwa na serikali.

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni sketi mbili nyeusi na blue bahari mpauko
ii. Mashati mawili meupe mikono mirefu.
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi
iv. Sare ya Michezo Kwa wasichana ni truck suti rangi ya blue.
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vi. Soksi jozi mbili nyeupe
vii. Sweta rangi ya blue bahari mpauko (*siyo lazima kuna joto)*
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) *rangi damu ya mzee drafuti ndogo mshono wa solo iwe ndefu hadi chini.*
ix. Tai mbili zenye kufanana na sketi yaani nyeusi na blue bahari mpauko
x. T-shirt rangi ya blue muundo wa form six yenye kola nyeupe

**<u>MUHIMU</u> : MAVAZI YOTE NUNUA HUKOHUKO AJE NAYO**

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari 07 ( Counter book 2Q )
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Godoro la kiwanafunzi futi 2.5
iv. Mashuka Jozi 2 rangi ya pink, blanket nyepesi 1 au shuka zito
v. Chandarua 1
vi. Nguo za dharura ( kitenge 1 na kanga 1 )
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
viii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko kwa matumizi yake mwenyewe.
ix. Kwanja 1 na Mfagio wa brash Brumu **( HGL NA HGFA )**
x. Jembe 1**, ( HGK )**
xi. Reki 1, **( HKL )**

**NB VIFAA HIVYO HAPA MADUKANI KIRANDO VIPO.**

**ANGALIZO KUHUSU**
**<u>MATIBABU</u> :**

**NI MUHIMU UMKATIE BIMA YA MATIBABU MWANAO**
**KURAHISISHA MATIBABNU YAKE ANAPOUGUA.**
**PIA HATUNA SPECIAL DIET**

## 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Fedha hii iwekwe kwenye akaunti ya shule**
**DEVELOPMENT KIRANDO SECONDARY SCHOOL**
**A/C 62001100059 NMB**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile,ikitokea amejisahau basi akifika akabidhi ofisini.**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kufuga ndevu;

vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule ERNEO C.MGINA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0754-530654 / 0624-530654 / 0779-530654 / 0684-829104**

- **Mwandamizi malezi (Matron ) 0762845392**



**ZINGATIA :**

NGUO ZIWE NDEFU IKIWA FUPI UTARUDIA KUSHONA NYINGINE.